**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

---

**31 MEI, 2018**

**1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1**

**2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018 ........................................................................................ 2**

2.1 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ........................................................................................ 3

2.1.1 Mgodi wa Dhahabu wa Buhemba ........................................................ 3

2.1.2 Chuo cha Madini Kampasi ya Nzega .................................................. 6

2.1.3 Mgodi wa Mchimbaji wa Kati (CATA Mining) ....................................... 7

2.2 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 ........................................................................................ 10

2.3 Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa Mwaka 2017/2018 ........................................................................................ 12

2.3.1 Madini ya Vito ya Tanzanite ,Almasi na Madini mengine ya Vito nchini ........................................................................................ 12

2.3.2 Madini ya Dhahabu ........................................................................ 15

2.3.3 Madini ya Ujenzi na Viwandani ........................................................ 17

2.3.4 Madini ya Bati ........................................................................ 18

2.3.5 Makaa ya Mawe ........................................................................ 20

**3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA ........................................................ 21**

3.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa fedha 2017/18 ........................................................................................ 22

3.2 Uchambuzi wa Taarifa ya hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina . 23

3.3 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati uliotolewa. ............................. 25

**4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA FUNGU 100 KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19 ............................................. 27**

4.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2018/2019....... 27

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato ............................................. 28

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ............................................. 29

**5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ........................................ 32**

**6.0 HITIMISHO ........................................................................................ 35**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa majukumu ya kikanuni Kamati ilifanya vikao kadhaa kwa lengo la kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na kufanya uchambuzi wa makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Pia Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; pamoja na miradi mingine inayosimamiwa na Wizara ya Madini. Lengo ni kujiridhisha na ufanisi wa utekelezaji miradi

hiyo pamoja na kuhakiki thamani ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inaonesha matokeo ya shughuli zilizotekelezwa katika kipindi tajwa pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Madini. Ziara hizo ilifanyika katika Mikoa ya Mara na Tabora (Nzega). Lengo la ziara ni kujionea Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, miradi iliyokaguliwa ni kama ifuatayo:-

i) Mgodi wa Dhahabu wa Buhemba

ii) Chuo cha Madini Kampasi ya Nzega

iii) Mgodi ya Wachimbaji wa Kati (CATA Mining)

## 2.1 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

### 2.1.1 Mgodi wa Dhahabu wa Buhemba

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yako ilifanya ukaguzi katika Mgodi unaomilikiwa na Serikali kupitia STAMICO wenye leseni ya utafiti (Prospecting Licence) namba PL 7132/2011 uliopo Wilayani Butiama, Mkoa wa Mara.

Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni uchenjuaji wa mabaki ya dhahabu yaliyoachwa katika kipindi cha Wakoloni na pili ni uchimbaji wa dhahabu katika Miamba migumu iliyothibitika kuwa na mashapo yenye **wakia 441,772 katika migodi ya 1, Buhemba, 4, Kilamongo South na Kilamongo North** baada ya kufanyika kwa upembuzi yakinifu katika Migodi hiyo ya wazi. Aidha, ukadiriaji wa mashapo katika mashimo ya Buhemba Main na Mwizi unaendelea kufanywa na Shirika letu la Madini kadri fedha zinavyoendelea kupatikana.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi huo Kamati ilielezwa kuwa, ili kuweza kutekeleza mradi huo jumla ya **Shilingi bilioni 8,936,337,023** zinahitajika, ambapo **Shilingi bilioni 6,421,081,912** zitatumika kununua mitambo ya uchimbaji na uchenjuaji na **Shilingi bilioni 2,515,255,111** kwa ajili ya gharama za uendeshaji katika kipindi cha miezi mitatu ya awali ya

utekelezaji wa mradi. Aidha, faida ya **Shilingi bilioni 15,655,197,502** inategemewa kutengenezwa kama fedha za uwekezaji zitapatikana.

**Mheshimiwa Spika**, toka Mwaka 2011 Mgodi ulivyokabidhiwa kwa STAMICO hakuna shughuli yoyote ile ya uchimbaji wala uchenjuaji iliyowahi kufanyika na sababu kubwa ikiwa ni ukosefu wa fedha kwa Shirika hilo pamoja na Mwekezaji atakayekubali kuwekeza katika Mgodi huo.

Aidha, Stamico kushindwa kuendeleza Mgodi huo kwa muda mrefu kumesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya Mgodi, upotevu wa vifaa na uvamizi mkubwa wa Wachimbaji wadogo wadogo katika eneo hilo hali ambayo inahatarisha sana usalama wa maisha yao.

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyo Migodi mingine inayomilikiwa na STAMICO kurithi madeni makubwa kutoka kwa wawekezaji waliofunga shughuli zao hapa nchini, pia Mgodi wa Buhemba unakabiliwa na deni la **Shilingi milioni 89,021,324** linalotokana na mapunjo ya mafao ya wafanyakazi wa zamani walioachishwa kazi mwaka 2007 wakati Mgodi huo unamilikiwa na Kampuni ya Meremeta.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashindwa kuelewa ni kwa nini Wawekezaji wanapofunga shughuli zao katika Migodi mingi hapa nchini wamekuwa wakiacha Madeni makubwa, ambayo hubebwa na STAMICO wanapokabidhiwa Migodi hiyo na Serikali. Aidha, sintofahamu ya Madeni hayo imeendelea kuwa mzigo kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuwa STAMICO hutakiwa kuyalipa Madeni hayo pale wanapokabidhiwa Migodi hiyo, pamoja na uwepo wa takwa la Kisheria la kuzingatia Wawekezaji wote wanapofunga shughuli zao wanaacha mazingira katika hali nzuri na Madeni yote yamelipwa hususani Kodi na Tozo mbalimbali za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto nyingine nyingi ambazo Kamati ilizibaini katika Mgodi huo ni dhahiri kuwa siyo rahisi kwa Serikali kupata faida kama itaamua kuwekeza. Aidha, uwekezaji huo utakuwa kama ule wa STAMIGOLD ambapo toka kuanzishwa kwake Mgodi huo haujawahi kutengeneza faida zaidi ya kutengeneza hasara (Madeni makubwa) ambayo yamekuwa mzigo mkubwa kwa Wizara ya Madini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara ya Madini kufanya tathmini upya ya Uwekezaji katika Migodi yote iliyorithiwa na STAMICO ili kuona kama kuna faida na sababu ya kuendelea na Uwekezaji huo. Ni vyema maeneo hayo

wakawapatia Wachimbaji wadogo na wa Kati ili waweze kuyaendeleza kuepusha migogoro isiyo ya lazima na wananchi wetu.

### 2.1.2 Chuo cha Madini Kampasi ya Nzega

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi katika chuo cha madini Kampasi ya Nzega, Mkoani Tabora lilipokuwa eneo la Mgodi wa Resolute. Eneo hili la Mgodi pamoja na rasilimali zake lilikabidhiwa rasmi kwa Chuo cha Madini tarehe 12 Disemba, 2014 kutoka kwa Kampuni ya uchimbaji madini ya Resolute (Tanzania) Ltd baada ya Kampuni hiyo kufunga shughuli za uzalishaji wa Madini.

**Mheshimiwa Spika,** Kampasi hii ilianzishwa mahsusi kwa ajili ya kutekeleza dhima na malengo ya Chuo cha Madini ambayo ni; kuongeza wataalam wa kada ya kati katika sekta ya Madini katika fani za Jiolojia na Utafutaji wa Madini, Uhandisi Uchimbaji na Uchenjuaji Madini, Usimamizi wa Mazingira Migodini na Upimaji wa Ardhi na Migodi.

Pili ilikuwa ni upanuzi wa Chuo hicho ili kiweze kuendesha shughuli zake kwa ufanisi zaidi kwa sababu ya uwepo wa migodi (*Pits*) ambayo itawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo. Na tatu ilikuwa ni kuifanya Kampasi ya Nzega kuwa

Kitovu cha Mafunzo (*Centre of Excellence*) kwa ajili ya kutoa mafunzo ya rasilimali za madini na mazingira kwa wachimbaji Wadogo Wadogo.

**Mheshimiwa Spika,** toka eneo hilo limekabidhiwa kwa Chuo hicho mwaka 2014 hakuna shughuli yoyote ile ya Kitaaluma iliyokwisha fanyika katika eneo hilo, pamoja na uwepo wa Miundo mbinu inayofaa kufundishia. Hali hiyo imesababisha eneo hilo kuvamiwa na Wachimbaji wadogo mara kwa mara hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa rasilimali na miundo mbinu ya chuo hicho.

**Mheshimikwa Spika,** kutokana na athari ya Mazingira iliyoachwa na mwekezaji wakati anafunga shughuli zake katika eneo hilo, ni vema Wizara ikakamilisha taratibu zote muhimu zinazotakiwa ili chuo hicho kiweze kukabidhiwa katika kitivo cha Uhandisi Migodi cha Chuo kikuu cha Dar Es Salaam ili kutimiza malengo mahsusi ya Chuo cha Madini.

### 2.1.3 Mgodi wa Mchimbaji wa Kati (CATA Mining)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi katika mgodi wa mchimbaji wa kati katika kijiji cha Kiabakari Mkoani Mara na kujionea uwekezaji katika Mgodi wa dhahabu wa Cata Mining. Mgodi huu unamilikiwa kwa ubia wa asilimia 50 kwa 50 kati ya

mtanzania na Mwekezaji kutoka Canada kupitia **leseni namba 483/2015** iliyotolewa mwaka 2014.

Mwaka 2015, CATA Mining iliingia makubaliano na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kuchenjua mabaki ya mchanga uliyoachwa na wachimbaji wa kikoloni na Novemba, 2016, Kampuni hiyo iliingia mkataba mwingine tena na Jeshi hilo kwa ajili kufanya utafiti wa Madini ya dhahabu katika mgodi wa Kiabakari kupitia leseni namba PL 10645/2015.

**Mheshimiwa Spika,** Mikataba yote miwili iliyoingiwa na pande hizi mbili ilikuwa na lengo la kugawana faida, ambapo hadi sasa JWTZ imelipwa jumla ya **Dola 690,550**, sawa na **Shilingi billioni 1.3** ikiwa ni sehemu ya makubaliano ya mkataba wa uchenjuaji wa mchanga (**Tailings**).

**Mheshimiwa Spika**, Mgodi huu unazalisha zaidi ya kilo **303.674** za dhahabu kwa Mwaka, na kulipa mrahaba jumla ya **shilingi 1.085 billion** pamoja na tozo mbalimbali zinazofikia jumla ya **shilingi bilioni 1.0.** Kampuni imekwishalipa jumla ya **Dola 529,000.00**, sawa **Shilingi 1,140,788,500/=,** kiasi ambacho kinashinda tenda ya Mgodi wa Kiabakari. Pia Mgodi huo umetoa ajira kwa Watanzania takribani 400 hususani Vijana wanaozunguka eneo hilo la Mgodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikishwa na sintofahamu inayoendelea kati ya JWTZ na Kampuni ya CATA Mining kupitia leseni namba PL 10645/2015. Kusimamisha uendelezaji wa leseni hiyo kwa katazo kutoka upande wa pili wa Mkataba huo ambaye ni JWTZ. Kitendo hicho ni kumnyima haki Mwekezaji huyo ambaye kimsingi alishafanya uwekezaji mkubwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka katika kwenye mabenki mbalimbali hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, **kwa kuwa;** toka awali JWTZ lilikubali kuingia Mkataba na Mwekezaji huyo kwa vigezo walivyokubaliana katika kuendeleza leseni hiyo, kusimamisha ghafla shughuli za uzalishaji za Mgodi huo imesababisha hasara kubwa kwa Mwekezaji kutokana na gharama alizokwisha ingia katika kuendeleza leseni hiyo.

**Na kwa Kuwa;** Sheria ya Madini Na. 14 ya Mwaka 2010 katika kifungu cha 95(1) a (v) inamzuia Mmiliki wa leseni ya Madini katika baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji Idhini/Kibali Maalumu kutoka kwa Mamlaka/Waziri mwenye dhamana na eneo hilo kumruhusu mtu huyo kuingia katika eneo hilo na kufanya shughuli zake kwa mujibu wa leseni yake.

Kwa msingi wa kifungu hicho JWTZ ilisharuhusu Mwekezaji huyo kuendeleza leseni hiyo katika eneo hilo kwa makubaliano ya

kugawana faida, Kamati inashauri kuwa Kuendelea kumzuia na kumsimamisha Mwekezaji huyo kufanya shughuli zake katika eneo hilo ni kumsababishia hasara ambazo kimsingi zinapunguza mapato ya Serikali na Halmashauri husika.

**Hivyo basi,** Ni vyema Ofisi ya Waziri Mkuu ikaingilia kati jambo hili kwa kuzikutanisha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Madini ili kupata ufumbuzi wa haraka wa kadhia hii, ambayo inatishia mwekezaji huyu kufilisiwa na mabenki kutokana na kushindwa kuendana na ratiba ya urejeshaji mikopo aliyochukua kuendeshea mgodi huu. Ikumbukwe kuwa mwekezaji huyu ameonesha kwa vitendo nia ya dhati kuwekeza na kuendeleza Sekta ya Madini kwa kulipa Kodi na tozo mbalimbali kwa Serikali pamoja na kuajiri Watanzania takribani 400 katika fani mbalimbali.

### 2.2 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia hali halisi ambayo Kamati iliona wakati wa Ukaguzi wa Miradi; inatoa ushauri kwamba:-

a) Kufanya tathmini upya ya Uwekezaji katika Migodi yote iliyorithiwa na STAMICO ili kuona kama kuna faida na sababu ya kuendelea na Uwekezaji huo. Kamati inaona ni vema maeneo hayo wakawapatia Wachimbaji wa Kati

ili waweze kuyaendeleza kuepusha migogoro isiyo ya lazima kwa wananchi;

b) Kutokana na athari ya Mazingira iliyoachwa na mwekezaji wa Mgodi wa Resolute wakati anafunga shughuli zake katika eneo hilo, ni vema Wizara ikakamilisha taratibu zote muhimu zinazotakiwa ili chuo hicho kiweze kukabidhiwa katika kitivo cha Uhandisi Migodi cha Chuo kikuu cha Dar Es Salaam ili kutimiza malengo mahsusi ya Chuo cha Madini, na

c) Ofisi ya Waziri Mkuu iingilie kati jambo hili kwa kuzikutanisha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Madini ili kupata ufumbuzi wa haraka wa kadhia hii, ambayo inatishia mwekezaji huyu kufilisiwa na mabenki kutokana na kushindwa kuendana na ratiba ya urejeshaji mikopo aliyochukua kuendeshea mgodi huu. Ikumbukwe kuwa mwekezaji huyu ameonesha kwa vitendo nia ya dhati kuwekeza na kuendeleza Sekta ya Madini kwa kulipa Kodi na tozo mbalimbali kwa Serikali pamoja na kuajiri Watanzania takribani 400 katika fani mbalimbali;

d) Upatikanaji wa fedha za kutosha kwenye miradi ya Maendeleo itaongeza kwa kiasi kikubwa makusanyo ya Maduhuli kama inavyotakiwa.

## 2.3 Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa Mwaka 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kazi zilizotekelezwa na Wizara ya Madini katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Februari, 2018 zilikuwa ni kuimarisha usimamizi na udhibiti wa rasilimali zetu kwa lengo la kuongeza makusanyo ya Maduhuli kwa Serikali. Kazi zilizotekelezwa na Idara ya Madini zilikuwa ni uthaminishaji wa Madini ya vito, usimamizi wa mnada wa Tanzanite pamoja na biashara ya Madini mbalimbali kama ifuatavyo;

### 2.3.1 Madini ya Vito ya Tanzanite ,Almasi na Madini mengine ya Vito nchini

#### (a) Madini ya Tanzanite

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza jitihada za Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwenye Sekta ya madini ya Vito hususani madini ya Tanzanite kwa maamuzi ya kizalendo ya kujenga Ukuta kuzunguka eneo la Mgodi wa Tanzanite (Mererani) zenye lengo la kuongeza udhibiti katika mfumo mzima wa biashara ya Tanzanite katika soko la ndani na la nje. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kusimamia biashara hii, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa madini haya

yanapata **Hati ya Uasilia** (Certificate of Origin) ilikuweza kudhibiti madini haya katika soko la nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua zilizochukuliwa na Serikali za kuendelea kudhibiti uholela uliokuwepo wa tanzanite katika soko la ndani na nje hali ambayo kimsingi inashusha thamani ya Tanzanite; Kwa mfano mnada uliyofanyika Disemba, 2017 ni **kilo 47 tu ndiyo zilizouzwa kati ya kilo 535.99 zilizochimbwa. Aidha, kilo 488.99 zimehifadhiwa katika Benki kuu tawi la Arusha pamoja na Maghala ya Mgodi ili kusubiri bei nzuri ya soko la Tanzanite.**

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kamati inashauri kuwa taratibu endelevu zinazoandaliwa na Wizara kuhusu Mnada wa Tanzanite zikamilishwe kwa haraka ili kuboresha Mnada huo ambao ndiyo tegemeo kubwa kwa wachimbaji na wafanyabiashara ya madini ya tanzanite. Mnada huu ukiratibiwa vizuri utaongeza tija ya uwepo wa madini haya hapa nchini.

**(b) Madini ya Almasi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza ushauri na maoni ya Kamati maalumu uliyoiunda ya kufuatilia mfumo mzima wa

biashara ya Madini ya Almasi hapa nchini, kwani baada ya kuimarisha usimamizi katika Mgodi wa Mwadui katika kipindi cha Julai hadi Februari, 2018 **Karati 3,047,784.56** zilizalishwa na **Karati 137,257.94** zilisafirishwa nje ya nchi. Almasi hiyo ilikuwa na thamani ya **Dola milioni 32,653,349.9** ni sawa na **Shilingi bilioni 72,921,000,000** na mrabaha wa **Dola za marekani milioni 2.25 sawa na Shilingi bilioni 5.02** ulilipwa Serikalini.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Wizara kutoa takwimu na taarifa zote za uzalishaji wa madini ya Almasi kutoka kwenye migodi mingine hapa nchini ili kujua mchango wake katika makusanyo ya Taifa letu.**

**(c) Madini mengine ya Vito**

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu ina utajiri mkubwa sana wa madini mengine ya vito kama vile **Rubi, Sapphire, Garnet, Tourmaline, Emerald, Scapolite, Tsavorite** pamoja na **Alexandrite** inayopatikana Wilayani Tunduru tu, aina hii ya madini ina thamani kubwa katika soko hivyo ni vema Wizara ikaweka utaratibu mzuri utakaowezesha kuchimbwa kwa Madini hayo ili yaweze kuchangia katika uchumi wetu.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Madini hajaweza kuripoti mchango wa Madini mengine ya Vito pamoja na uwepo wake katika Mikoa yote nchini. **Kamati inaishauri Wizara kuwa, taarifa zote za Madini yanayozalishwa nchini zinapatikana ili kujua mchango wa Madini hayo katika makusanyo ya Serikali.**


### 2.3.2 Madini ya Dhahabu

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Februari, 2018 jumla ya kilo 31,450 sawa na **Wakia milioni 1.01** zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi na migodi yote mikubwa na ya Kati hapa nchini, uzalishaji huu umepungua kwa **asilimia 28** kutoka Wakia **milioni 1.42** zilizozalishwa mwaka 2016 pamoja na Wakia **milioni 1.36** zilizozalishwa mwaka 2015.

***Kielelezo Na.1 Kinafafanua zaidi kuhusu uzalishaji wa madini ya Dhahabu nchini.***

| Mwaka | Wakia(Milioni) |
|---|---|
| **2017** | **1.01** |
| **2016** | **1.42** |
| **2015** | **1.36** |

***Chanzo: Taarifa za Wizara na usanifu wa Kamati***




***Chanzo: Taarifa za Wizara na usanifu wa Kamati***

**Kushuka kwa uzalishaji wa Madini haya kumechangia pia kushuka kwa makusanyo ya malipo ya Mrabaha wa awali kulinganisha na miaka iliyopita.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitishwa na mchango hafifu kutoka kwa Wachimbaji wadogo kwenye makusanyo ya Mrabaha pamoja na Serikali kutoa ruzuku kwa baadhi ya Wachimbaji Wadogo ambapo mnufaika wa chini alipata **Dola za Marekani elfu 50,000** sawa na takribani **Shilingi milioni 100,000,000** na mnufaika wa juu alipata **Dola za Marekani 100,000** sawa na takribani **Shilingi milioni 200,000,000** kwa kila mchimbaji katika awamu zote mbili.

**Mheshimiwa Spika, katika taarifa za makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi tajwa hakuna mchango wa Wachimbaji wadogo uliopatikana katika makusanyo ya Mrabaha. Aidha, kukosekana kwa taarifa za uzalishaji wao ni ishara tosha kuwa Madini haya huuzwa katika Soko lisilo rasmi na hivyo kushindwa kuwanufaisha Wachimbaji wenyewe na Serikali kwa ujumla. Kamati inaitaka Wizara kuimarisha usimamizi kwa Wachimbaji wadogo ili kuhakikisha kuwa Madini yote yanayozalishwa yanaingia katika mfumo rasmi wa ulipaji wa kodi za Serikali ili na wao wachangie katika pato la Taifa kama yalivyo malengo ya Wizara hii.**

2.3.3 **Madini ya Ujenzi na Viwandani**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi na makusanyo kidogo tunayopata kama nchi kutoka kwenye madini ya Ujenzi na Viwandani, jumla ya **Shilingi bilioni 1.62** tu za Mrabaha zililipwa Serikalini pamoja na uwepo wa madini hayo kwa wingi hapa nchini. Aidha, Kamati hairidhishwi na uwekezaji usiyo na tija unaofanywa na STAMICO kwa kushindwa kuhodhi soko la madini hayo ili kuongeza Makusanyo kama inavyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, **Kamati inaishauri Wizara kuwa, kama STAMICO inashindwa kuendeleza Migodi ya Madini ya Ujenzi kama ule wa Ubena Zomozi ni vema wakapewa Wananchi wenye nia ya kuendeleza Migodi hiyo na STAMICO ikabaki na**

**kazi ya kutoa ushauri wa kitaalam na Serikali ikabaki na kazi yake ya kukusanya Mapato.**

2.3.4 **Madini ya Bati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitishwa na sababu zinazotolewa na Wizara ya Madini za kushindwa kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Bati kwa ukosefu wa fedha za mtaji wa kununulia mtambo wa kuchakata bati pamoja na ukosefu wa Hati ya uasilia yaani **(ICGLR Certificate of Origin)** inayosababisha Madini hayo kushindwa kuuzwa nje ya nchi.


**Mheshimiwa Spika,** Changamoto zinazotolewa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kimsingi siyo changamoto ambazo wameshindwa kuzipatia ufumbuzi kama Shirika na Wizara yenye dhamana ya madini nchini. Kamati inaona kuwa kusimama kwa mradi huo siyo kutokana na ukosefu wa mtaji kama inavyoripotiwa bali ni kukosekana kwa utashi wa Serikali wa kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Madini hayo yenye soko kubwa kwa nchi jirani ya Rwanda.

Aidha, fedha za Mtaji wa kuendesha mradi huo takribani **Shilingi bilioni 1.57** zilikuwepo na kutumika kununulia tani **106.267** za Bati kutoka kwa wachimbaji wadogo na kuhifadhia katika ghala. **Hata hivyo; dhamira ya kuanzisha Kampuni tanzu ya *Kyerwa Tin Company* imeshindwa kutimia**

**na kuwasababishia hasara Wachimbaji wadogo waliohamasishwa katika uzalishaji na tayari wamewekeza katika uzalishaji wa Madini hayo.**

**Mheshimiwa Spika,** Wakati Serikali ikiendelea kusuasua katika uendelezaji wa Mradi huo, taarifa za Benki ya Dunia kuhusu soko la Madini haya zimeonesha kuwa, bei ya Madini ya Bati inatarajiwa kupanda kutoka **Dola 20,225/MT (Metric Tone**) kwa Mwaka 2017 hadi kufikia **Dola 20,834/ MT** ifikapo mwaka 2020. Aidha, bei ya Madini hayo itaendelea kuimarika na kupanda katika kipindi cha miaka mitano ijayo, na ifikapo Mwaka 2030 inatarajiwa kuwa imepanda hadi kufikia **Dola 23,000/MT.**

**Kielelezo Na. 2 kinaonesha mwenendo wa Bei ya Madini ya Bati Duniani.**



**Hivyo basi, Wizara ya Madini iweke mpango Mkakati wa kiuwekezaji kwa ajili ya kuendeleza Mradi huu wa Madini ya Bati kwa kuwa taarifa za Benki ya Dunia zinaonesha wazi fedha ambazo nchi yetu itazipata kutokana kuimarika kwa soko la Madini hayo Duniani.**

### 2.3.5 **Makaa ya Mawe**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haioni nia ya dhati ya Serikali ya kuendeleza Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira kwa kushindwa kupeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu jumla ya **Shilingi bilioni 10,000,000,000** kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbalimbali za Mgodi huo. Pamoja na uhitaji mkubwa wa Makaa hayo katika Viwanda mbalimbali hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 jumla ya **tani 2,477** zimezalishwa zenye thamani ya **Shilingi milioni 158,528,000.** Takribani mwaka mzima sasa Makaa hayo hayajaweza kuuzwa kutokana na sababu mbalimbali zilizoelezwa na STAMICO kuwa ni ukosefu wa Miundo mbinu ya barabra. **Kamati inashauri Wizara ya Madini kushirikiana na Halmashauri husika pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili ziweze kutengeneza barabara hiyo ambayo ni ya muhimu sana kwa ustawi na maendeleo ya Mgodi pamoja na Halmashauri hiyo.**

**Mheshimiwa Spika**, Mgodi wa makaa ya mawe wa Ngaka umeendelea kufanya shughuli za uzalishaji ambapo jumla ya **tani 340,295** zilizalishwa na kuuzwa zenye thamani ya Dola za marekani milioni 15,500,000 ambapo Serikali ililipwa mrabaha wa jumla ya **Dola za Marekani 466,345.48**.

Kamati inashauri Wizara kuwa ni vema sasa wakafanya maamuzi ya dhati kabisa ya kuwekeza kwenye Miradi ambayo uhitaji wake katika soko la ndani umeongezeka zaidi baada ya zuio la Serikali la uingizaji wa Malighafi hizo kutoka nje. Aidha, ni matumaini ya Kamati kuwa, kama uwekezaji huo utafanyika utaongeza makusanyo ya Serikali hasa mrabaha.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha uzalendo wake katika kulinda rasilimali zetu za Madini ambazo zilikuwa hazilinufaishi Taifa ipasavyo kwa kuunda Tume ya Madini ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia ipasavyo maendeleo ya Sekta hii ya Madini nchini.**

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018;

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kushughulikia mambo mengi ya kibajeti ya Wizara ya Madini, Kamati yako ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/18 katika maeneo yafuatayo:-

a. Makusanyo ya Maduhuli;
b. Hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina; pamoja na
c. Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati uliotolewa.

### 3.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa fedha 2017/18

**Mheshimiwa Spika**; Wizara ya Madini ilipanga kukusanya Maduhuli jumla ya **Shilingi bilioni 194,397,098,763** kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2018 jumla ya Maduhuli ya **Shilingi bilioni 200,685,683,840** zilikusanywa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya Wizara ya Madini, ongezeko hili ni sawa na **asilimia 103** ya lengo waliojiwekea kwa mwaka wa fedha 2017/18. Zifuatazo ni Sababu zilizoelezwa na Wizara kuchangia kuongeza kwa Makusanyo ya Maduhuli;

(a) Kuimarika kwa udhibiti wa utoroshaji wa madini kwa kushirikiana na vyombo vya Serikali;
(b) Kuongezwa kwa viwango vya mrabaha kutoka asilimia 4 hadi asilima 6 kwa madini ya metali, na kutoka asilimia 5 kwenda 6 kwa madini ya vito; na
(c) Kuanzishwa kwa tozo ya ukaguzi asilimia 1 ya mauzo ya madini.

**Mheshimiwa spika,** Ongezeko hili la ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni ishara tosha kwa Kamati na Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Madini

imejitahidi kuimarisha usimamizi na uangalizi wa rasilimali zetu kitu ambacho kilikuwa ni kero na aibu kubwa kwa Taifa letu. Kamati inaamini kuwa Sekta ya Madini sasa itakwenda kutoa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kama inavyotarajiwa na Wananchi wetu.

### 3.2 Uchambuzi wa Taarifa ya hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina


**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliidhinisha jumla ya **shilingi 998,337,759,500** kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini, kati ya fedha hizo **shilingi 52,445,367,000** ilikuwa ni kwa ajili ya Idara ya Madini. Kati ya **shilingi 21,783,000,000** sawa na **asilimia 41.53** ilikuwa kwa ajili ya Miradi ya maendeleo. Aidha, **Shilingi bilioni 30,662,367,000** sawa na **asilimia 58.47** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2018 iliyokuwa Idara ya Madini ambayo ndiyo Wizara ya Madini sasa ilikuwa imepokea **Shilingi bilioni 15,670,239,173** ambayo ni sawa na **asilimia 13.69** ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa fedha 2017/18, kiwango hicho cha fedha kilikuwa katika mgawanyo ufuatao; fedha za Miradi ya Maendeleo zimepokelewa **Shilingi** milioni **834,976,618,** sawa na **asilimia 3.83** ya Bateji iliyotengwa na **shilingi bilioni 6,723,898,405** sawa na **asilimia 51** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi**

**bilioni 8,111,364,150** sawa na **asilimia 51** kwa ajili ya mishahara**.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitishwa na utolewaji wa fedha za miradi usiyoridhisha kwani hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2018 Wizara ya Madini imepokea **asilimia 3.83** tu ya bajeti iliyodhinishwa kwa ajili ya maendeleo, hali hii inakwamisha kwa kiasi kikubwa miradi ya maendeleo ambayo kimsingi ndiyo tunayoitegemea katika kuongeza ukusanyaji wa Mapato ya ndani kwa Wizara hii. Miradi iliyokwamishwa na upatikanaji huu wa fedha usiyoridhisha ni; Mradi wa Kiwira, Kabulo, Mradi wa Ununuzi wa Bati, Mradi wa Dhahabu Buhemba, Mrdai wa uchimbaji wa kokoto na Mradi wa STAMIGOLD.

**Kielelezo Na. 3 ni ufafanuzi wa utolewaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo pamoja na Matumizi ya Kawaida**




***Chanzo: usanifu wa Kamati na Randama ya Wizara 2018/19***

Mwenendo huu wa utolewaji wa fedha kutoka Hazina unapunguza kabisa ufanisi wa Wizara hii mpya ambayo sisi kama Taifa tunatarajia mengi kutoka kwao katika usimamizi wa rasilimali za Madini ambazo kwa muda mrefu tumekuwa hatunufaiki nazo.

### 3.3 **Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati uliotolewa.**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti pamoja na usimamizi wa Miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka husika. Hata hivyo, baadhi ya Maoni na Ushauri

uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado haujafanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo-:

a) Serikali kutopeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwenye miradi ya kimkakati kama vile Kiwira kunachelewesha utekelezaji wa miradi hiyo yenye tija kwa maendeleo ya viwanda hapa nchini.

b) Kamati bado hairidhishwi na ufuatiliaji mdogo unaofanywa na Wizara kwa Wabadhilifu wa Ruzuku zilizotolewa na Serikali katika awamu zote mbili zilizotolewa mwaka 2014/15. Ufuatiliaji huo wa kusuasua umeshindwa kuwachukulia hatua watu wote waliokiuka matumizi ya fedha hizo za umma; na

c) Serikali kupitia Wizara ya Madini bado inashindwa kuwasaidia Wachimbaji wa Kati ambao kimsingi wameonekana kuwa ndiyo wawekezaji wazawa ambao wameweza kuisimamia na kuendeleza sekta ya madini kwa manufaa makubwa, kwa mfano mgodi wa Busolwa Mining bado unakabiliwa na changamoto ya uhaba wa eneo la Mgodi pamoja na kutoa ajira kwa vijana wengi pamoja na mchango wake mkubwa kwa Serikali na jamii inayouzunguka kuliko hata Migodi ya Wawekezaji wakubwa.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA FUNGU 100 KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

### 4.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19, Kamati imebaini kuwa malengo yaliyowekwa na Wizara yakiweza kusimamiwa ipasavyo Wizara itaweza kufikia Dira iliyojiwekea yakuwa ; **Wizara inayoheshimika Afrika katika kuendeleza rasilimali za madini ili ziweze kuchangia kwa ufanisi katika uchumi wa Taifa na ustawi wa Watanzani.**

**Mheshimiwa Spika,** Wananchi na Taifa kwa ujumla tuna imani kubwa sana na Wizara ya Madini kuwa itaweza kuiweka Tanzania kwenye ramani ya Dunia ya kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa Madini na kwamba Wizara hii itasimamia vyema rasilimali za madini nchini ili ziweze kulinufaisha Taifa kupitia usimamizi mzuri wa Sheria, Kanuni na Malengo Makuu sita(6) Wizara iliyojiwekea. Malengo hayo ni haya yafuatayo:-

a) Kuboresha huduma kwa waathirika na kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;

b) Kuimarisha na kuendeleza Mkakati wa Taifa na Mpango wa kupambana na Rushwa;
c) Kuboresha utoaji huduma kwa Wadau wa Sekta ya Madini;
d) Kuongeza Mchango wa sekta ya Madini kijamii na kiuchumi;
e) Kuwaimarisha Wachimbaji wadogo wadogo wa Madini nchini; na
f) Kuimarisha mifumo ya ukaguzi na usimamizi wa migodi

**Mheshimiwa Spika,** Uwepo wa Sheria mpya za *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, The Natural Wealth and Contracts (Review and Re- Negotiation of Unconscionable Terms)* na Marekebisho ya Sheria ya Madini zilizopitishwa na Bunge lako tukufu mwaka 2017 pamoja na kuanzishwa kwa Tume ya Madini nchini itasaidia usimamizi mzuri wa rasilimali zetu.

## 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Makisio ya makusanyo ya Maduhuli yanakadiriwa kuwa jumla ya **Shilingi bilioni 321,672,507,000** kwa mwaka wa fedha 2018/19 ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 194,397,098,763** zilizokadiriwa kukusanywa kwa Mwaka 2017/18. Ongezeko hili ni sawa na **asilimia 60.84.**

Kati ya makusanyo yote kwa mwaka wa fedha 2018/19 **Shilingi bilioni 310,598,007,000** sawa na **asilimia 99.34** zitawasilishwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, **Shilingi bilioni 2,074,500,000** sawa na **asilimia 0.66** zitatumika kwa ajili ya kuendeshea shughuli za Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Ongezeko la makusanyo haya limetokana na ongezeko la malipo ya viwango vipya vya Mrabaha kwenye Madini ya Metali, Vito na kuanzishwa kwa tozo ya ukaguzi wa mauzo ya madini, Kamati yako inaishauri Wizara kubuni vyanzo vingine mbadala vya mapato ambavyo vitakuwa ni endelevu kutokana na rasilimali zilizopo katika Wizara hiyo ikiwa ni pamoja na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa kutumia Wataalamu walionao katika chuo cha Madini.

### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2018/19 Wizara ya Madini imeomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 58,908,481,992** ikilinganishwa na **shilingi bilioni 52,445,367,000** zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2017/18. Bajeti hii imeongezeka kwa **asilimia 11.** Ongezeko hili la bajeti limetokana na uwepo wa Tume ya Madini ambayo inatarajia kuongeza watumishi wengine wapya kwa ajili ya kutekeleza majukumu mapya ya Tume hiyo. **Kamati inasisitiza**

**Serikali kuhakikisha fedha zinatoka kwa wakati ili Tume hii yenye majukumu makubwa iweze kutekeleza majukumu yake kama inavyotarajiwa.**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 19,620,964,000** sawa na **asilimia 32** ya Bajeti yote kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 21,783,000,000** zilizotengwa mwaka 2017/18, Bajeti hii imepungua kwa **asilimia 9.93**. Katika bajeti hiyo ya maendeleo **Shilingi bilioni 16,800,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2,820,964,000** ni fedha za nje. Aidha, **Shilingi bilioni 17,700,000,000** sawa na **asilimia 90.21** zitaelekezwa kwenye miradi ya Kimkakati. Kamati inaipongeza Wizara kuendelea kupunguza utegemezi wa fedha za nje kwenye Bajeti ya Miradi ya maendeleo.

Pamoja na ongezeko la **asilimia 11** ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2018/19 kwa Wizara hii, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo imepungua kitu ambacho Kamati inaona kitaathri utekelezaji wa miradi hiyo, ambayo katika Bajeti ya 2017/18 haikupelekewa fedha pamoja na Bunge kuidhinisha fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yako hairidhishwi na mwenendo wa Serikali kuendelea kutenga fedha kidogo katika miradi ya

Kimkakati ambayo inahitaji fedha nyingi kama vile Miradi wa Makaa ya Mawe Kiwira na Kabulo. Miradi hii ili iweze kuanza uzalishaji wenye tija ambao tunautarajia kama Taifa zinahitajika fedha za kutosha nyingi zaidi ya zilizotengwa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa, kwa kuwa fedha hizo zilizotengwa kwa ajili ya Mradi wa Kabulo hazitatosha kukidhi uzalishaji wenye tija ni bora zikaelekezwa katika mradi mwingine kama vile Mradi wa Kokoto ili uweze kuongeza uzalishaji na kisha kuongeza makusanyo ya Wizara ya Madini.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imetenga **Shilingi bilioni 39,287,517,992** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na **asilimia 66.69** ya bajeti yote, ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 21,783,000,000** kwa mwaka wa fedha 2017/18. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida imeongezeka kwa **asilimia 44** ukilinganisha na mwaka 2017/18. Aidha, kati ya fedha hiyo **Shilingi 20,953,262,992** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo(OC) na **Shilingi bilioni 18,334,255,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** Ongezeko hili la bajeti ya Matumizi Mengineyo na bajeti ya Mishahara kwa Wizara hii ni kutokana na kuanzishwa rasmi kwa Wizara ya Madini pamoja na

kuanzishwa kwa Tume ya Madini ambayo nayo inatarajiwa kuajiri watumishi wengi pamoja na kufungua Ofisi za Mikoa. **Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa fedha zitakazo idhinishwa na Bunge lako tukufu kwa Wizara hii mpya zinatolewa kwa wakati ili Wizara pamoja na Tume ya Madini waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kama inavyotarajiwa na Wananchi.**

## 5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yako imetekeleza majukumu yake ya msingi yaliyoainishwa katika Kanuni ya 98 (1) na (2) pamoja na kanuni ya 117(11) a Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Hivyo basi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara ya Madini;

5.1 Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kuharakisha ufuatiliaji wa fedha za Ruzuku zilizotolewa na Serikali kwa Wachimbaji Wadogo wadogo katika awamu zote mbili, Pia Wizara ihakikishe inafanya upembuzi yakinifu kabla ya kutoa rukuzu awamu nyingine ili kuepuka changamoto zilizojitokeza katika awamu zilizotangulia.

5.2 Kamati hairidhishwi na mwenendo wa utekelezaji wa shughuli za Mgodi wa STAMIGOLD kwa sababu lengo la kuanzishwa kwa Mgodi huo limeshindwa kutimia na badala yake

umekuwa ukizalisha Madeni makubwa takribani bilioni 60 sasa. Wizara iangalie namna bora ya kuendesha mgodi huo au kuufunga kama itaona inafaa kwa maslahi ya Taifa kuliko kuendelea na uzalishaji usiyo na faida.

5.3 Kamati inaitaka Wizara ya Madini kufanya tathmini na kujiridhisha kama kweli kuna faida tutakayoipata kama nchi tukiwekeza fedha **Shilingi bilioni 8.6** zinazoombwa kwa ajili ya kuendeleza Mgodi wa Buhemba, ilhali hakuna faida tuliyopata mpaka sasa katika uwekezaji uliofanyika katika Mgodi wa STAMIGOLD zaidi ya kuzalisha madeni makubwa ambayo ni mzigo kwa Serikali.

5.4 Kamati inaona ni vema Mgodi wa Buhemba na ule wa STAMIGOLD wapewe wachimbaji wa Kati wenye nia ya kuuendeleza, hii itakuza sekta ya wachimbaji wa Kati nchini ambao wameonesha kuwa na mchango mkubwa katika makusanyo ya mapato na Serikali ikabaki kwenye ukusanyaji wa mapato tu.

5.5 Kamati inaendelea kuishauri tena Wizara kupitia upya Mkataba wa Ubia kati ya STAMICO na TANZAM 2000 uliongia mwaka 2011 kuendeleza Mgodi wa Buckreef, kwa kuwa Mkataba huo umedhihirisha kutokuwa na manufaa ya kiuchumi katika uendelezaji wa Mgodi huo licha ya uwepo wa Mashapo yenye uhakika wa kuzalisha dhahabu na kuliingizia Taifa mapato.

5.6 Pamoja na makusanyo ya Mrabaha kuongezeka kwa mwaka wa fedha 2017/18 hususani katika idara ya Madini, Kamati hairidhishwi na uendelezaji wa Wachimbaji wa Kati ambao wana mchango mkubwa katika makusanyo ya Wizara. **Hivyo basi, Kamati inashauri Wizara kuwa ili kuongeza makusanyo hayo ni vema Wawekezaji hawa wazawa wakasaidiwa kupata ufumbuzi wa haraka kuhusu kero zinazowakabili. Hii itavutia Wawekezaji Wazawa kuendeleza sekta hii kuliko kusubiri wawekezaji toka nje ambao ndiyo wanaofaidi misamaha ya Kodi mbalimbali.**

5.7 Kwa kuwa miradi ya Makaa ya mawe imeonekana kuwa na mchango unaoridhisha kwenye makusanyo ya Mrabaha takribani **Dola za Marekani 466,345** zilipatikana kutokana na mauzo ya makaa ya mawe katika Mgodi wa Ngaka. **Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa; miradi yote ya Makaa ya Mawe ni vyema Serikali ikatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza Miradi hiyo, kwa kuwa uhitaji wa malighafi hiyo ni mkubwa sana hapa nchi baada ya zuio la Serikali la kuagiza Makaa hayo toka nje ya nchi.**

5.8 Wizara ya Madini iweke mpango Mkakati wa kiuwekezaji kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Madini ya Bati kwa kuwa taarifa za Benki ya Dunia zinaonesha wazi, fedha ambazo nchi yetu

itazipata kutokana na kuimarika kwa Soko la Madini hayo Duniani.

5.9 Wizara kuangalia upya Mikataba yote tuliyoingia na Wawekezaji wanaowekeza katika uchimbaji wa Makaa ya Mawe ili kujiridhisha kama nchi inafaidika na uwepo wa Kampuni hizo katika uendelezaji wa Makaa hayo.

5.10 Serikali iangalie namna bora ya kuwezesha Wakala wa Jiolojia nchini ili iweze kufanya tafiti za madini yote nchini nakuwa na **Kanzi data** ambayo itatumiwa na Wawekezaji toka nje, hii itapunguza athari kubwa za kimazingira zinazosababishwa na Watafiti kutoka nje ya nchi ambao wakimaliza tafiti zao nchi hainufaiki na tafiti zilizofanywa kwenye rasilimali zake.

5.11 Wizara ibuni na kuwa na mikakati endelevu ya vyanzo vingine vipya vya ukusanyaji wa Mapato kuliko kutegemea tozo za Madini pekee, kwani ikitokea uzalishaji wa Madini umeshuka Wizara itakosa mapato tunayoyatarajia kama nchi.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwa umahiri wao waliouonesha wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Wajumbe hawa wamefanyakazi kwa ari kubwa na hatimaye

kukamilisha Taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hawa kwa majina yao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Dustan Luka Kitandula, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb - Mjumbe
11. Mhe. John Wegesa Heche, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Rashid Ajari Akbar, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Yosepher Ferdinand Komba, Mb - Mjumbe
19. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb - Mjumbe

25. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** nitoe pia shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mhe. Angellah Kairuki, (Mb) – Waziri wa Madini, pamoja na Manaibu Waziri wa Madini Mhe. Stanslaus Nyongo, (Mb) na Mhe. Doto Biteko, (Mb) pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Simon Msanjila kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Steven Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Mwanahamisi Munkunda na Ndg. Felister Mgonja pamoja na Msaidizi wa Kamati ndg. Grace Mwenye kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100 Wizara ya Madini kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo ni **Shilingi Bilioni 58,908,481,992**.

**Mheshimiwa Spika**, Naunga mkono hoja na Naomba kuwasilisha.

Dunstan Luka Kitandula

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

**31 Mei, 2018**